

SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR

Namba Yetu:

Maulizo: 024 2238321

Dharura: 024 2230232



Afisi Kuu:

S. L. P: 235,

Zanzibar - Tanzania

Simu: +255 24 230 237 / 8

Simu: +255 774 334 455

Simu Pepe: +255 24 223 1906

Barua Pepe: info@zeco.co.tz

TAARIFA YA UTOAJI WA HUDUMA YA USAJILI KATIKA VITUO VYA GAMBA NA MAKUNDUCHI

Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) limeanza rasmin utaratibu wa usajili katika hatua ya awali ya kuunga umeme katika vituo vya Gamba na Makunduchi.

Vituo hivyo vya kanda ambavyo vinahudumia Mkoa wa Kaskazini kwa kile kilichopo Gamba na Mkoa wa Kusini kwa kile kilichopo Makunduchi vimeanza kutoa huduma hiyo kuanzia tarehe 15 Novemba, 2021 katika kuwaondolea wananchi wa mikoa hiyo usumbufu wa kuifuata huduma ya usajili Mjini.

Awali vituo hivyo vilikuwa vinatoa huduma za ununuzi wa umeme na huduma za dharura kwa wananchi wa mikoa hiyo ambapo sasa vimeongezewa huduma ya usajili baada ya kukamilika kwa uwekaji wa mfumo "system" wa utoaji wa huduma hiyo.

Malengo ya Shirika kwa siku za usoni ni kutoa huduma zote ambazo zinatolewa Makao Makuu ikiwemo huduma za uunganishaji umeme na kuongezewa nguvu zaidi katika utatuzi wa matatizo ya wateja.

Vituo vya umeme Gamba na Makunduchi vilianza kurejesha huduma zake rasmin Januari, 2013 baada ya kusitisha utoaji wa huduma mnamo miaka ya 1986 kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo ya uchakavu wa miundo mbinu yake.

Vituo hivi, vilijengwa mwishoni mwa miaka ya 1960 na kuanza kazi mwanzoni mwa miaka ya 1970 kwa lengo la kutoa huduma katika nyumba za maendeleo zilizojengwa Gamba na Makunduchi.

Hatua ya ujenzi wa vituo hivi ilikuwa ni katika adhama ya utekelezaji wa ilani ya chama cha ASP ya kuwaletea wananchi wote maendeleo mijini na vijijini ikiwa ni lengo la Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964.

**Imetolewa na;
Kitengo cha Mawasiliano na Huduma kwa Wateja
Shirika la Umeme (ZECO)
Zanzibar.**

Mawasiliano: *Mawasiliano yote ya barua yapelekwe kwa Meneja Mkuu
Tunastahiki kukupa huduma bora, wakati ukihakikisha unasawazisha bili yako ya umeme kwa wakati"*
Mkuu wa Mawasiliano 0773926914